

Muhtasari


- Wakulima katika ukanda unaopata mvua mara mbili kwa mwaka wanashauriwa kupanda mazao hususan katika maeneo yenye unyevunyevu unaoweza kuotesha mbegu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia njia bora katika uandaaji mashamba, uvunaji na uchaguaji wa mbegu bora za kupanda katika maeneo yenye unyevunyevu wa ziada hususan maeneo ya mabondeni.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 01-10, 2020

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali hiyo ilisababisha kutokea kwa vipindi vifupi vya migandamizo midogo ya hewa. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani lilikuwepo katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilipelekea upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 01-10, 2020

Mifumo ya hali ya hewa ilichangia uwepo wa mvua katika maeneo mengi nchini kama inavyoonekana katika kielelezo. Kiwango cha mvua kuanzia milimita 51 hadi milimita 200 kilirekodiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, maeneo machache ya Morogoro kusini, mashariki mwa Mtwara, na mashariki wa Dar es Salaam yalirekodi mvua zaidi ya milimita 201, vile vile kiwango hicho kilirekodiwa katika maeneo ya magharibi mwa Moshi, kaskazini mwa Kigoma na kaskazini mwa Lindi. Pia, kiwango cha chini cha mvua cha kuanzia milimita 50, kimeweza kurekodiwa katika maeneo ya kusini mwa Ruvuma na Mtwara.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 01- 10, 2020.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 01-10, 2020

Katika dikadi hii, maeneo mengi yanayopata mvua mara moja kwa mwaka, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kuelekea kukomaa na wakulima walikuwa wakijihusisha na shughuli ya palizi. Katika mkoa wa Mbeya, wakulima walikuwa wanapanda maharagwe. Pia katika mikoa ya Njombe na Iringa kuliripotiwa uvunaji wa viazi mbatata. Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wakulima waliendelea na uandaaji wa mashamba na kuanza kupanda. Katika mikoa ya Simiyu na Kagera, wakulima walikuwa wanapanda mahindi na maharagwe, katika kipindi hicho hicho baadhi ya maeneo waliendelea na uvunaji wa mahindi yaliyopandwa mwishoni mwa msimu wa mvua za vuli. Maeneo machache ya ukanda wa pwani ya kaskazini (Morogoro, Tanga, na visiwa vya Pemba, na Unguja) zao la mpunga lilikuwa

katika hatua ya kutoa maua. Mkoani mwanza iliripotiwa kuwa zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kuchomoza wakati katika mikoa ya kanda ya kati (Dodoma na Singida) mahindi yalikuwa katika hatua ya ubebaji.

Kwa ujumla katika kipindi hiki, maeneo mengi ya nchi iliripotiwa kuwepo kwa unyevunyevu wa kutosha kwa ajili ya ukuaji wa mazao na malisho, ingawaje mkoa wa Mtwara kuliripotiwa kuwepo kwa ukavu katika baadhi ya maeneo.

**HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA
MACHI 01-10, 2020**

Kiwango cha maji katika mabwawa na utiririkaji katika mito viliimarika katika maeneo mengi ya nchi.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA
KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2020**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali hiyo inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa vipindi vifupi vya migandamizo midogo ya hewa. Joto la bahari la juu kidogo hadi juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo hafifu kuvuma kutoka magharibi hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Mifumo ya upepo katika tabaka la chini na tabaka la juu haina mchango mkubwa katika mifumo ya utengenezaji wa mvua katika nchi yetu.

**HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI
CHA MACHI 11-20, 2020**

Maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria (Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), Mikoa ya magharibi mwa nchi (Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) na Mikoa ya pwani ya kusini

(Mtwara na Lindi) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo. Katika Mikoa ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajia kuwepo kwa vipindi vya mvua katika maeneo machache wakati pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajia kuwepo kwa mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache hususan nusu ya kwanza ya dekadhi hii. Katika ukanda wa kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) na nyanda za juu Kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

**HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2020**

Mvua za msimu (masika) zilizoanza katika maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka kunauwezekano wa kuchangia ongezeko la unyevunyevu katika ardhi na kusaidia katika upandaji na ukuaji wa mazao na malisho. Katika kipindi hiki, wakulima wanashauriwa kutumia mvua hidhi za msimu wa masika kupandia mzao hususan katika maeneo yenye unyevunyevu wa kutosha kuoteshea mbegu. Vile vile, wakulima wanashauriwa kutumia njia bora za utayarishaji mashamba, uvunaji na uchaguaji wa mbegu za kupanda katika maeneo yenye unyevunyevu mwingi hususan mashamba yaliyopo katika mabonde. Matarajio ya kuwepo kwa mvua katika ukanda unaopata mvua mara moja kwa mwaka zitaboresha unyevunyevu katika aridhi na kusaidia ukuaji wa mazao kama vile maharagwe na mihogo. Hata hivyo, wakulima na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

**HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI
CHA MACHI 11-20, 2020**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuimarika katika maeneo mengi ya nchi hususan katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz;

Tovuti: www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania